

Yehova Amwimarisha Gideoni

WAAMUZI SURA 6-7

WAISRAELI WALIKUWA NA MAISHA MAGUMU.
WAMIDIANI WALIENDELEA KUWAVAMIA WAISRAELI.
WAMIDIANI WALIWANYANYASA WAISRAELI, WALIWAPIGA
NA KUHARIBU MASHAMBA YAO.

WAISRAELI WALIMWOMBA
YEHOVA AWASAIIDIE.

MUNGU AKAMTUMA MALAIKA
WAKE ILI AMTEMBELEE
MWANAMUME ANAYEITWA GIDEONI.


YEHOVA,
TAFADHALI
TUOKOE!

MIMI?
MIMI SI KITU.
NINAWEZAJE
KUOKOA ISRAELI?

YEHOVA
YUPO PAMOJA NAWE,
EE MWANAMUME
SHUJAA NA MWENYE
NGUVU. **UTAWAOKOA**
ISRAELI.

KWA SABABU
YEHOVA ATAKUWA
PAMOJA NAWE.

ILI KUJUA IKIWA GIDEONI ALIMWAMINI YEHOVA
KWA MOYO WAKE WOTE, YEHOVA ALIMPA MGAWO
WA PEKEE WA KUJARIBU **SANAMU YA KIPAGANI**.



WAKATI WA USIKU GIDEONI AKAWACHUKUA
WANAUME KUMI NA KWENDA **KUONDOA SANAMU**.

HATA HIVYO WAISRAELI BADO WALIKUWA
HATARINI! MAJESHI YA WAMIDIANI NA MENGINE
YALIVUKA MPAKA WA ISRAELI NA KUPIGA KAMBI
KATIKA NCHI TAMBARARE YA CHINI YA YEZREELI.

TUMEINGIA
KATIKA ENEO LAO.
SASA **HAKUNA** CHA
KUTUZUIA!

HAWATUWEZI!

GIDEONI ALIMWOMBA YEHOVA AMPE ISHARA
ITAKAYOONYESHA **KWAMBA ATAWASAIKIA**.
BASI, YEHOVA AKAFANYA **MIUJIZA** MIWILI YENYE
KUSTAAJABISHA. (SOMA WAAMUZI 6:36-40.)



GIDEONI NA WANAJESHI WAKE
WAKAJITAYARISHA ILI KUPIGANA NA
WAMIDIANI.

IKIWA
TUTAFUATA MAAGIZO
YA YEHOVA,
ATATUSAIDIA
TUSHINDE!

KISHA YEHOVA AKAONGEA NA GIDEONI.

GIDEONI,
KATI YA WANAJESHI
WAKO JASIRI NI 300 TU
WATAKAOPIGANA. NDIPO
UTAKAPOJUA KWAMBA **MIMI**
NDIYE NILIOKOA ISRAELI.



TUTATUMIA
MBINU GANI
KUPIGANA?


KILA MMOJA
WETU ATACHUKUA
BARAGUMU, MTUNGI,
NA MWENGE.

KISHA
TUTAFANYA KAMA
GIDEONI
ANAVYOFANYA.

YEHOVA
YUKO PAMOJA NASI!
KATIKATI YA USIKU, PIGA
BARAGUMU, VUNJA-VUNJA
MITUNGI, NA PAAZA
SAUTI . . .







WAMIDIANI WANAKIMBIA, NA WAISRAELI WANAWAKIMBIZA. INGAWA JESHI LA ISRAELI LILIZIDIWA KWA UWIANO WA ASKARI-JESHI 1 MWISRAELI KWA ASKARI-JESHI 450 WA ADUI, YEHOVA ALIWASAIIDIA KUSHINDA VITA.

TUNAJIFUNZA NINI KUTOKANA NA HADITHI HII?

KWA NINI GIDEONI ALIWAOGOPA WAMIDIANI?

DOKEZO: WAAMUZI 6:2-6, 15.

GIDEONI ALIFANYA NINI ILI KUPATA UJASIRI?

DOKEZO: WAAMUZI 6:27a, 36-40.

UNaweza JINSI GANI KUPATA UJASIRI UKIWA NA HOFU?

DOKEZO: ZABURI 138:3, 8; METHALI 17:17; WAEBRANIA 13:6.